# MWONGOZO WA KUSAHIHISHA KARATASI YA 102/2

# KIDATO CHA NNE MUHULA 2 2024

## 1. UFAHAMU

**a) adha za msimulizi**

i) **kutengana** na familia yake ( baba na mama)

ii) **kufiwa** na nyanya yake mpenzi

iii) **hofu** ya ardhi alikomzika nyanya yake kunyakuliwa

iv) kufanya **vibarua** akiwa na umri mdogo

v) **kulala** katika mazingira mabovu ingawa yeye ni mtoto/ kulala chini ya michai/kwenye saruji/sokoni

vi) **makazi** duni ya wafadhili wake yanayomfanya kutoka na kwnda kuatafuta makazi mbadala

***( za kwanza 5 x 1 = 5) kadiria majibu ya mwanafunzi***

b) **mzigo wa mwenzio ni kanda la usufi**

Msimulizi anasema wanawake wa siku hizi hawana moyo wa kumlea mwana wa mwenzao kwa kuchelea ugwe uliowaunganisha baba na mama mtoto utamea tena. ***( 1x 2=2)***

c) **methali**

kitanda usichokilalia hujui kunguni wake ***( 1x1)***

d) **kinaya – (ukoloni mamboleo**)

i) mashamba katika nchi hii yangali yanamilikiwa na wazungu

ii) familia ya Richard ingali inamiliki shamba la michai na mibuni

iii) wazungu kumiliki mashirika ya utengenezaji mazao yaa mimea kamamajanichai n kahawa nchini

iv) Kining'inya wa Richard ( mlowezi) kuwa ndiye Afisa Mkuu Mtendaji wa Shirika hilo.

e) **Msimulizi ni mkamavu**

i) anaondoka kwenda kutafuta makazi bila kujua aendako

ii) anafanya kazi kama vile kuchuna chai ili aweze kujikimu

iii) anakataa kumtegemea shangazi yake kwani tayari alikuwa na mzigo wa kugharamia masomo yake.

***( zozote 2x1)***

f) i) nilipiga moyo konde – nilijituliza/nilijiliwaza

ii) kadhia – mkasa ***(2x 1 =2 )***

Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

## 2. UFUPISHO

a)

i) Walio na bidii mwishowe hufanikiwa na kufurahia matunda yao
ii) Waliofaulu hufanyika kielezo kwa watu wengi
iii) Watu wengi waliofaulu katika historia ni wale waliojituma katika masomo na majukumu yao
iv) Ben Carson ni mmoja wa watu waliofaulu maishani licha ya kuwa alizaliwa katika familia yenye changamoto
v) Daktari James Mwangi amewasaidia maelfu ya wananfunzi kote nchini kupitia '*Wings to Fly'*
vi) Wanaonufaika na mradi huu hujiunga na vyuo maarufu duniani
vii) Hao hulipiwa karo yote, hupewa masurufu kila wakati na nauli kila wanapoenda au kutoka shuleni.
viii) Benki hufanya hivyo ili kuwaonyesha wanafunzi umhimu wa kufanya bidii masomoni.
ix) Nchi hii ingekuwa na watu kumi wenye maono kama ya James mwangi ingeendelea sana.

***( zozote 7x 1)***

**b)**

i) Wakfu wa Jomo Kenyatta Foundation vilevile huimaarisha masomo ya wanafunzi werevu kutoka familia zisizojiweza
ii) Huwalipia wanafunzi karo na mahiaji mengine
iii) Mashirika mengine kama vile Brookside , kampuni ya Milo na Coca Cola pia huchangia kuendeleza elimu
iv) Kampuni hizi kuchangia kudhamini michezo baina ya shule
v) Kusudi lao kufanya vile ni kuhimiza bidii katika kukuza vipawa
vi) Vipawa huhitaji bidii kwani wenye bidii ndio hufaidika mwishowe.
vii) Wanafunzi wengi wajizatiti masommoni na michezoni ili kupaa hatimaye. Wanafunzi kutoka familia maskini wajiamini na watie bidii masomoni
viii) Wakifanya hivi wataonekana na wafadhili hawa na maisha yao kufanikiwa hatimaye
ix) Bidii ni muhimu katika ufanisi wa maisha ya baadaye. **( zozote 6x1 =6)**

M
**a - 7**
**b – 6**
**Ut - 2**
**15**

**ADHABU YA MAKOSA**

**6H = ALAMA 3**

**6 S = ALAMA 3**

**Z = baada ya maneno ya kwanza 10, alama 1, kila baada ya maneno 5, ½**

Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

## 3. MATUMIZI YA LUGHA

a) linda **1/0**

b) m - chwe - o

K - KKI - I **1/0**

c) i) ’Ala

ii) A’ la! **2x1**

d) Mtoto alikuwa akilia akienda shuleni. **2/0**

e) Wanafunzi **walilala** walipomsikia mwalimu **akitoka** darasani. **(2x1)**

f) Chakula hakikuwa kimepikwa na mama. **2/0**

g) wenyewe ulikatika vibaya./ zenyewe zilikatika vibaya. **2/0**

h) nyua za shule zetu zitakarabatiwa upya. **2/0**

i) D[1/2] audi:[1/2] T[1/2] utafumumukana baada ya ibaada.[1/2] **(4x ½ )**

j) Nilifurahia baada ya kumsalimia rais. **1/0**

k) mkulima – yambwa tendewa/ shamirsho kitondo

shamba lake – yambwa tendwa

uma – ala

kwa uma - chagizo

jana – chagizo **(yambwa zozote 2x 1, chagizo yoyote 1x1 )**

l) rafiki – mwandani/ mhibu/ somo/sahibu/swahibu/bui/mbasi/msiri

mvulana – ghulamu

hasira – ghadhabu/ghaidhi/hamaki/mafutu/maya/fundo **3x1**

m)

| S | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| KN | | KT | | | | |
| N | S | T | N | V | H | N |
| Wahunzi | waliokuwa kiwandani juzi | walilipwa | mishahara | yao | kwa | hundi. |

**(KN – 2, KT – 2)**

n) wachezaji – mazoea/ unominishaji

walijistarehesha – kujirejelea/kijifanyia kitendo wenyewe

o) kwao – wataenda wanakomiliki wazee hao wenyewe

kwao – wataenda kwa watu wengine **2x1**

Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

p) **wia** - Kazi hiyo iliniwia nyepesi ndipo nikaimaliza haraka. **1x2**

| q) | wa - | li - | o - | f - | iw - | a | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | nafsi/ngeli | wakati | kirejeshi | mzizi | kauli | kiishio | **6 x ½ = 3** |

r) ebo/pakacha/nobe/po/ng'o – dharau

barabara/sadakta/haya/ewaa/sawa/ndiyo/naam/taib/hasa – kukubaliana na jambo **2 x 1**

s) vyovyote vizuri – kirai nomino

vitakubalika – kirai tenzi

baada ya kununua gari jipya – kirai husishi

gari jipya – kirai nomino

kununua gari jipya – kirai tenzi ***vyovyote 4 x ½ = 4***

**Adhabu ya makosa 6h = alama 3**

**Sarufi > ½ ya alama alizopata katika kijisehemu**

## 4. ISIMUJAMII

a) sajili ya matangazo/ sajili ya matangazo ya michezo **1x2**

i) b) matumizi ya msamiati maalum – mechi/goal/refarii/nyani
ii) lugha yenye kuchanganya ndimi – amepiga miss
iii) lugha yenye urudiaji/takriri – anaenda, anaenda ...
iv) lugha inayoibua taharuki hasa mchezaji anapokaribia kufunga bao – ndiye huyooooo… hatari kwenye lango…
v) matumizi ya lugha hisishi – salaaaaale!
vi) Lugha ya kijazanda/ kistiari – nyani – kumaanisha mlinda lango
vii) Matumizi ya chuku – golkipa ameona moto wa bluu
*viii)* Lugha legevu – anapotaja majina ya wachezaji ili kudumisha kasi ya mchezo- Masimba, Masimba, wananyang'anywa, *Pedro, Giroud,kante*
ix) Matumizi ya lakabu – Masimba
x) Lugha ya kusifu – huyu Kante ni moto kama pasi ya umeme…
xi) Lugha yenye misimu – golaa, refa ***( kadiria za kwanza 8 x1 )***

**Adhabu ya makosa**

**4h x ½ = *2 h***

***4s x ½ = 2 s***

Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes